035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

   Jibu sahihi ni **D**

   **Katika karatasi ya majibu:**

   **2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa:-***

Malezi ni________1__________aliyopewa kila kiumbe na Mola. Hakuna kiumbe________2________ anayejifungua mtoto na kisha kutompenda au kukosa_______3__________.Huruma ya mzazi na mapenzi yake_________4___________ mwana ndiyo inayotupa methali, uchungu wa mwana aujuaye mzazi. Suala nyeti ni hili: mbona tunaona watoto wakiteswa? Mateso_____5__________ukatili wa kukiuka mipaka umeshamiri. Kila uchao ripoti za magazeti na rungoya zinaeleza_____6________vya kung'oa roho za watu______7___watoto wakichomwa moto au kutandikwa______8__________kuzirai. Tabia_________9___________za kinyama zinatokana na nini jamani? Mtoto_______10__________yule anahitaji kuongozwa na_______11________vizuri.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. zoezi | B. wajibu | C. jukumu | D. dhima |
| **2.** | A. yeyote | B. chochote | C. wowote | D. vyovyote |
| **3.** | A. kumdunisha | B. kumdhamini | C. kumthamini | D. kumhudumu |
| **4.** | A. ya | B. kwa | C. kwenye | D. katika |
| **5.** | A. kama | B. kwa | C. ingawa | D. kwenye |
| **6.** | A. viza | B. matukio | C. vicha | D. visa |
| **7.** | A. za | B. kwa | C. vya | D. cha |
| **8.** | A. hadi | B. ama | C. lau | D. ilhali |
| **9.** | A. hii | B. hizi | C. hayo | D. zizi |
| **10.** | A. lau | B. mithili | C. iwapo | D. kama |
| **11.** | A. kutelekezwa | B. kuelekezwa | C. kukemewa | D. kulewa |

Mwanafunzi ________12___________ na mwenye ________13__________ huwafurahisha walimu wake.Anapoipanga kazi yake _________14_________ hupata usaidizi unaomwelekeza kuliko wale________15_____________ tu .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **12.** | A. msafi | B. safu | C. safi | D. safika |
| **13.** | A. adhabu | B. athabu | C. adha | D.adabu |
| **14.** | A. mzuri | B. vizuri | C. wazuri | D. zuri |
| **15.** | A. wanaoandika | B. wanaandika | C. wanaojiandika | D. wanaojiandikia |

**_Kutoka swali 16 hadi 30, jibu maswali kulingana na maagizo:-_**

**16**. "Ki" imetumikaje katika sentensi:

Mwalimu wetu hufundisha akiandika.

A. Kuonyesha hali ya kuendelea.
B. Kuonyesha hali ya kufuatana kwa matendo.
C. Kuonyesha hali ya mazoea.
D. Kuonyesha hali ya matukio kutendeka pamoja.

**17.** Chagua jibu lisilo sahihi:

A. Bonde ni sehemu ya ardhi baina ya vilima viwili.
B. Kilele ni sehemu ya juu ya mlima.
C. Kisiwa ni sehemu kubwa ya ardhi iliyoingia baharini.
D. Chemchemi ni mahali maji yanapobubujika.

**18.** Geuza katika usemi taarifa:

"Ukisoma kwa bidii utafua dafu mwaka huu," mwalimu alimwambia mwanafunzi.

A. Mwalimu alimwambia mwanafunzi kuwa angesoma kwa bidii angefua dafu mwaka huo.
B. Mwalimu alimwambia mwanafunzi kuwa angesoma kwa bidii atafua dafu mwaka huo.
C. Mwalimu alimwambia mwanafunzi kuwa akisoma kwa bidii angefua dafu mwaka huo.
D. Mwalimu alimwambia mwanafunzi kuwa angesoma kwa bidii angefua dafu mwaka huu.

**19.** Kivumishi '-a' unganifu kimetumikaje katika sentensi ifuatayo?

Nyumba ya udongo haihimili vishindo.

A. kuonyesha kumiliki.
B. Kuonyesha aina.
C. kuonyesha hali.
D. kuonyesha matumizi.

**20** Milioni moja mia tisa sitini na tisa elfu , mia nane thelathini na nane kwa tarakimu ni :

A. 1,969,388
B. 1,969,883
C. 1,969,838
D. 1,696,838

**21.** Chagua jawabu sahihi:

Baba ________________ mgeni wake mpaka langoni.

A. alimsindikisha
B. alimsindikiza
C. aliendanisha
D. alimtolesha

**22.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi.

A. Mtu huyu ni fisadi lakini yule ni mwadilifu.
B. Maskanini mwangu mmenadhifishwa na kitwana.
C. Gari la kwanza limefika kwenye stendi mapema.
D. Mgeni atawasili mnamo saa saba adhuhuri.

**23.** Mtaalamu anayehusika na uwekaji wa hesabu za pesa ni

A. mwekahazina
B. mshenga
C. mhasibu
D. hamali

**24.** Chagua sentensi iliyotumia kielezi kiigizi.

A. Alhamdulilahi! Maulana ameninusuru.
B. Mwogeleaji alitumbukia majini chubwi!
C. Unapovamiwa na nyuki sharti ulale kifudifudi.
D. Tunafaa kuishi kistaarabu daima.

**25.** 'Na' imetumikaje katika sentensi ifuatayo:
Juma ana homa ya matumbo.
A. Kuonyesha hali ya kumiliki.
B. Kuonyesha kiunganishi.
C. Kuonyesha kuchanganya.
D. Kuonyesha hali fulani.

**26.** Chagua sentensi iliyotumia kihisishi kifaacho.
A.Huree! Tumefeli mtihani wa mwisho.
B. Pukachaka! Ametoa jibu mwafaka.
C. Ah! Leo baridi imeniathiri mno.
D. Pole rafiki! Mtoto wako amepona.

**27.** Mariamu alipokuwa akielekea nyumbani macheo, aligundua kuwa kivuli chake kilikuwa nyuma yake. Je, alikuwa akitoka upande gani?
A. Mashariki
B. Magharibi
C. Kaskazini
D. Kusini

**28.** Kiungo cha mwili kinachosafisha damu ni:
A. ini
B. figo
C. pafu
D. moyo

**29.** Chagua ukanusho ufaao wa sentensi:
Uchaguzi utafanywa baadaye mwaka huu.
A.Uchaguzi hutafanywa baadaye mwaka huu.
B. Uchaguzi hautafanywa baadaye mwaka huo.
C. Uchaguzi hutafanywa mwanzoni mwaka huo.
D. Uchaguzi hautafanywa baadaye mwaka huu.

**30.** Kinyume cha methali: "Haba na haba hujaza kibaba' ni:
A. Tembe na tembe ni mkate.
B. Maji ya kifuu bahari ya chungu.
C. Chovya chovya humaliza buyu la asali.
D. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40:-***

Kati ya wasia muhimu tuliousiwa na babu zetu ni ule usemao, "Kuuliza si ujinga." Hawakukomea hapo, walisema, "Aulizaye ataka kujua." Huo nao haukuwa mwisho wa nasaha zao. Walinena, "Atangaye sana na jua hujua. Atafutaye hachoki, akichoka keshapata." Lakini wenye roho ngumu kama paka hawajali kuyakumbuka hayo.

Kwa nini katika darasa, wanafunzi wengine huonekana werevu na wepesi wa kuelewa mambo wanayofundishwa upesi kuliko wengine? Ni kwa sababu huwa wanauliza walimu mambo yoyote ambayo hawayaelewi vizuri. Hawapendi kusimama mlangoni bila kubisha ngo! ngo! ngo!

Kwa nini Fatuma na Omari wanaendelea kukielewa Kiswahili vizuri na kukichangamkia hivyo? Ni kwa kuwa hawaogopi kuuliza maswali. Jambo usilolijua ni usiku wa giza totoro. Ukishauliza ukaelezwa utapata mwangaza mweupe pepepe! Aliye katika mwangaza huangaza. Aha! Apelekaye mkono kutamalaki si kazi.

Ajabu ni kwamba wanafunzi wengine, wenzao wanapouliza maswali darasani, wao huwacheka kwakwakwa! Nao hao wachekaji si lolote si chochote ila ni domokaya tu! Hawawi wengine ila ni wale wale akina yahe wanaoshika mkia darasani katika mtihani. Wanafunzi hodari wanaopenda kuuliza maswali, hushangaa na kustaajabu mno wanapowasikia wenzao wakicheka hadi mbavu kuwauma eti kwa sababu wamesikia swali likiulizwa darasani. La ajabu ni lipi kama si umbeya na uzumbukuku tu? Mwanafunzi bora hujifunza kila wakati na kila mahali. Aidha hujifunza kutokana na maswali ya wenzake. Shabash! Haba na haba hujaza kibaba.

Kilele cha ajabu ni kwamba mwalimu ametoa kazi ya ziada wanafunzi wakaifanyie nyumbani au katika muda wao wa ziada baada ya masomo darasani. Maseki, Matheka, Kitheka, Onyiero, Mwakicheko, Kenua na Menonje, wote ni wanafunzi wasiojali kuuliza maswali. Kwao, kuuliza ni kicheko. Kufika wakati wa kuzifanya kazi hizo za ziada, hawana habari. Hawajui wafanye nini. Hatimaye wataanza kufanya kazi shaghalabaghala bila msingi. Wengine hawana mwao wafanye maswali hadi nambari ngapi. Kwa nini? Hawaulizi! Ni ujinga mkubwa kutouliza. Yakini tunajua dhahiri shahiri kuwa kuuliza si ujinga. Kutouliza ndio ujinga. Uliza ujibiwe. Uliza upate kujua.

**31.** Kwa nini kutouliza ni ujinga? Kwa sababu
A. usipouliza utakuwa mjinga zaidi.
B. asiyeuliza hajui kitu.
C. wajinga huwa hawaulizi maswali.
D. asiyeuliza hawezi kujua na atadumu na kutojua kwake.

**32.** Nasaha bora kama za methali aghalabu zina faida.
A. kwa wanaozizingatia maishani.
B. na hasara kwa wanaouliza maswali.
C. zikitumiwa wakati wa kuuliza maswali.
D. kwa kila mtu aulizaye na asiyeuliza.

**33**. "Apelekaye mkono kutamalaki si kazi," ni sawa na methali
A.Mwomba chumvi huombea chunguche.
B. Mwomba Mungu hachoki.
C. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
D. Mbio za sakafuni huishia ukingoni.

**34.** Wanafunzi wanaoonekana kufahamu mambo barabara darasani daima ni
A. waliokuja kusoma na kujifunza.
B. wanaofundishwa vizuri kwa umakinifu.
C. wale aghalabu huuliza maswali bila kuyaonea haya.
D. wale aghalabu husoma kwa bidii na utulivu.

**35.** "Ukibisha hodi utafunguliwa" ni sawa na kusema
A. ukiuliza utajua
B. ukiambiwa utaelewa
C. ukiuliza utajibiwa
D. ukiita utaitikiwa

**36**. Kutojua jambo kumelinganishwa na
A. kucheka kwakwakwa!
B. domokaya
C. weupe wa mwangaza
D. giza totoro

**37.** Uchunguzi umeonyesha kwamba wanafunzi wanaowacheka wenzao darasani wanapouliza maswali daima ndio
A. werevu zaidi wasiohitaji kuuliza maswali.
B. wanaosoma zaidi kuliko wengine.
C. wenye akili tambuzi wanaoelewa mambo upesi.
D. zumbukuku wasiojua kwamba kuuliza ni kujifunza.

**38.** Orodha ipi ni ya wanafunzi wasiofadika na methali "Kuuliza si ujinga"?
A. Nyokabi, Omari
B. Mwakicheko, Menonje, Maseki
C. Onyiero, Omari, Matheka
D. Kitheka, Nyokabi, Kenua

**39.** Kinyume cha wanaoshika mkia ni
A. wanaoshika usukani.
B. wanaoshika zamu.
C. wanaoshika tama.
D. wanaoshika nanga.

**40.** Taarifa hii inamhimiza mwanafunzi
A. achelee kuuliza maswali yoyote anapoona kuna umuhimu.
B. asichelee kuuliza maswali popote anapoona kuna umuhimu.
C. anyamaze ajifunze anapowasikia wengine wakiuliza maswali.
D. awasaidie wenzake kuuliza maswali badala ya kucheka ovyo.

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50:-***

Tata alijiona sasa ni kijana aliyebaleghe. Akaona ni wakati wa kujichagulia mwenyewe kati ya makuruhu na ahasani. Jambo la kwanza lililomjia akilini lilikuwa kutafuta njia ya kujitenga na aila yake. Sio kujitenga kiasi cha ardhi na mbingu lakini alitaka akae peke yake ili aweze kujiamulia alitakalo bila ya kubugudhiwa na mtu. Alichoshwa kabisa na kazi za nyumbani. Mikono yake ilikuwa imetoa dasi kwa kamba ya kisima na miguu yake sugu na kovu kwa kutafuta kuni mwituni. Tena kulikuwa na kundi la mbuzi la kupeleka malishoni na konde la mpunga kuwinga ndege. Hata hivyo, kilichomfika kooni zaidi yalikuwa matusi ya wazee wake.

Tata alikuwa amekwisha amua kuondoka. Tatizo sasa lilikuwa aondoke aelekee wapi? Ni katika hali hiyo ndipo anasa na shamrashamra za mjini zilimjia. Alikumbuka kinaganaga hali ilivyokuwa mjini wakati alipowahi kuuzuru. Kila kitu cha mjini kilianisi. Alikumbuka kuwaona waliovalia mavazi ya kuanisi wakati huu kwenye magari ya kifahari. Nyuso zao zilijaa bashasha.

Bustani za starehe zilikuwa kila mahali. Muziki mwanana uliotoka katika bustani ungewatoa nyoka pangoni. Licha ya yote kulikuwa pia na majumba marefu ya kuvutia yaliyojengwa kwa ustadi. Alipogutuka kutoka kumbukumbu yake, alibaini jambo la kufanya mara moja. Angeifunga safari

yake moja kwa moja hadi kwa rafiki yake Sijali. Sijali alikuwa sahibu yake mkubwa walipokuwa shuleni pamoja kabla ya kwenda mjini.

Tata hakutaka cha lile wala hili. Siku iliyofuata, asubuhi na mapema, alitwaa virago vyake muhimu akaviweka katika mkoba na kufunga safari. Wahenga hawakukosea waliponena kuwamsafiri ni aliye bandarini. Alipofika kwenye kituo cha mabasi aliabiri basi moja tayari kung'oa nanga.

Alijaribu kujikumbusha mambo moyo wake ulipoanza kumdunda kwa kasi mara ilipoonekana wazi kuwa baada ya kusafiri kwa muda angekuwa mjini. 'Baada ya kutoka kituo cha mabasi, pana mkahawa halafu alifuata njia kubwa iliyokuwa mkono wa kushoto. Kisha soko la mboga halafu kitu kipi? 'Je, atapotea?' . . . Ukweli wa mambo ni kwamba, alianza kushikwa na jakamoyo. Hata hivyo, alipiga moyo konde. Yakini maji ukiyavulia nguo huna budi kuyaoga.

Alipofika mjini hali ilikuwa tofauti kabisa. Kitu cha kwanza alichokitafuta kilikuwa mkahawa. Hakuuona. "Uko wapi?" Alishangaa. Akiwa bado katika hali hiyo ya kustaajabu, alijikuta amepigwa kumbo na mtu asiyemjua. Alishikwa na vuguto. Kila upande alioutazama aliwaona watu wamefurika furifuri. "Ah, watu hawa wote wanaelekea wapi? Alishangaa. Hakujua kabisa la kufanya. Lakini alikuwa na hakika, hakuweza kuona mkahawa aliokuwa akitafuta.

**41**. Kwa nini Tata alijiona kuwa yeye ni barobaro?

A. Alichoshwa kabisa na kazi za nyumbani.
B. Alikuwa ameona mengi.
C. Matusi ya wazee wake.
D. Alikuwa na uwezo wa kujiamulia.

**42**. Kwa nini mikono ya Tata iliota dasi kwa kamba ya kisima?

A. Alikuwa anateka maji kutoka kisimani.
B. Alikuwa anavuta maji kutoka kisimani.
C. Alikuwa anakokota maji.
D. Alikuwa akibeba maji kutoka kisimani.

**43**. Ni kweli kusema

A. Tata alikuwa kijana wa kike.
B. Tata alifanyishwa kazi za kijungumeko nyumbani.
C. Tata alikuwa ametembelea mjini hapo awali.
D. Muziki uliotoka bustanini uliwatoa nyoka pangoni.

**44.** Kulingana na taarifa, jambo lililomkera sana Tata ni

A. kuwinga ndege shambani.
B. matukano ya wazazi.
C. kupotea mjini.
D. kupeleka mbuzi machungani.

**45.** Je, ni maisha gani Tata aliyotarajia kuyapata mjini?

A. yenye buraha na furaha.

B. ya kujikwatua na sifa.

C. yenye uhaba na taabu.

D. ya shamrashamra na fedheha.

**46**. Maana ya msemo piga kumbo ni

A. kumsukuma mtu.

B. kumshambulia mtu.

C. kaba shingoni kwa mkono.

D. kumtega mtu.

**47.** Nini maana ya kumbukumbu kulingana na aya ya tatu?

A. vitu vizuri vya wakati uliopita.

B. fikira zinazopita akilini mwa kiumbe.

C. mawazo ya matukio ya awali akilini mwa mja.

D. marejeo ya matukio ya dhahania.

**48.** "Msafiri ni aliye bandarini." Methali hii inamaanisha

A. tusichelewe kulikabili na kulitatua tatizo.

B. ukitaka kusafiri itakubidi uende bandarini.

C. ni muhimu kuzingatia mawaidha tunayopewa tusitaabike baadaye.

D. ni muhimu kufanya mambo mapema badala ya kungojea hadi mwisho.

**49.** Tata alipowasili mjini

A. alifanikiwa kwenda kwa rafikiye, Sijali.

B. alipotea njia ya kwenda kwa rafikiye.

C. aliporwa vitu na watu waliofurika furifuri.

D. alishangazwa na kubomolewa kwa mkahawa alioujua.

**50**. Chagua kichwa mwafaka cha ufahamu huu.

A. Masaibu ya Tata.

B. Masahibu ya Tata.

C. Tata na Sijali.

D. Safari ya mjini.

*Umepewa dakika 40 kuandika insha yako*

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Endeleza insha hii:

Mawingu meusi yalitanda angani na ghafla matone mazito mazito ya mvua ........................................................................................